**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI NDAGO – IRAMBA MKOA WA SINGIDA

**OFISI YA RAIS,**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI NDAGO**

S.L.P 60,
KIOMBOI-IRAMBA
26/4/2024

MKUU WA SHULE: PRISCA T. MDEMU
Simu: **0759018542/0774712099**
**MWALIMU MWANDAMIZI TAALUMA: 0735249569**

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI:
…………………………………………………………………………..

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NDAGO, HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA MKOA WA SINGIDA**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule ya sekondari **NDAGO** iliyopo Wilaya ya **Iramba** katika Mkoa wa **Singida** mwaka **2024** katika Tahasusi ya HGL/HKL. **KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI NDAGO.**
2. Shule iko kilometa 55 kutoka Singida mjini. Kama utapanda gari toka MBEYA, Dar Es Salaam, Arusha au Iringa Utashukia Singida mjini na kisha panda bajaji Kwenda stendi ya **UKOMBOZI** na upande gari za **NDAGO** na ushukie **Ndago Sekondari.**
3. Kama utapanda basi la moja kwa moja toka MWANZA, BUKOBA, SHINYANGA, TABORA kueleke Sweta hivoa Dar Es Salaam na mabasi yote yenye uelekeo wa Kwenda Dodoma, Morogoro, Mbeya (barabara ya kati) atashuka kituo kinachoitwa **MISIGIRI**, na hapo atapanda gari ndogo aina ya HIACE/Noah ni umbali wa kilomita ishirini na tano (25M) mpaka kufika Shuleni.
4. Muhula wa masomo utaanza **1/7/2024** kama ilivyotangazwa kwenye vyombo vya Habari na Wizara inayoshughulikia masuala ya Elimu.
   Aidha una muda mrefu wa kumuandaa mtoto hakuna sababu ya kuchelewa kuripoti shule! Ninasisitiza mwanafunzi afike shuleni mapema tarehe husika muda wa kuripoti ni kuanzia **saa mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na moja na nusu jioni.** Kama kuna dharura tumia namba za shule kuutarifu uongozi.

**MAHITAJI MUHIMU YA KUZINGATIA**

2.1 SARE YA SHULE

a) Sare ya shule ni sketi 2 za draft (Chocolate brown na Nyeupe) kitambaa Kizito cha suti grade 1, sketi mbili (2), mshono wa rinda bapa (rinda box) kwa ajili ya ufanano kwa wale watakao kosa sketi hizo basi hata shuleni anaweza kuzipata kwa gharama ya shilingi 30,000 kwa sketi moja.
b) Mashati mawili meupe ya mikono mirefu. ( Aje nayo)
c) Wanafunzi wanaovaa hijabu (kijuba) iwe nyeupe na ndefu kufika usawa wa nyonga, na hijabu zote ziwe za kitambaa cheupe aina ya babi au halua (sio kitambaa cha mpira au aina nyingine)
d) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi, Jozi mbili (2)
e) Sare ya michezo ni T-shirt rangi ya blue, raba rangi nyeupe (jozi moja) na traki suti rangi ya kijivu (jozi moja)
f) Soksi nyeupe kuanzia jozi mbili

g) Sweta la **chocolate brown** yenye shepu ya V mbele – shingoni, kwa watakaokosa Sweta hizo shuleni pia zinapatikana kwa Bei ya tsh 15,000)
h) Nguo za kushindia (shamba dress) sketi nyeusi moja au mbili marinda ya kupanga (mbele marinda nane au saba na nyuma vivyo hivyo) jumla marinda 16 au 14, iwe ndefu mpaka chini kama sketi ya darasani.
i) Aje na Tisheti mbili za kushindia rangi ya kijivu kwa wale watakao kosa aje na shilingi elfu 30 (TSHS 30,000) zinapatikana shuleni)
j) Nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa isipokuwa aje na kanga/vitenge jozi moja tu, atatumia wakati wa kuoga.
k) Aidha Ndago Sekondari kuna baridi, hivyo mwanafunzi anaweza kununua pull neck (sweta la kaba shingo) NYEUPE ya kuvalia ndani ya shati la shule.

**2:2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo:**

i. Madaftari makubwa (counter book quire 4) madaftari nane na madaftari ya msomi madogo 8 kwa ajili ya majaribio ya ndani.
ii. **Ream (A4)** Mbili (2) kwa ajili ya shughuli za Kitaaluma.
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iv. Scientific Calculator kwa wanafunzi wanaosoma Geography.
v. Godoro la sponji futi 2.5 inch 4 na mto wa kulalia
vi. Mashuka Jozi 2. (light blue 1 na Pink 1) na foronya zake, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 (*nyeupe);*
vii. Nguo za ndani za kutosha na taulo za kike za kutosha
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko na dumu la lita tano la kuhifadhia maji ya kunywa
x. Jembe moja lenye mpini na ufagio mmoja mlaini (soft broom) na chelewa kwa kila mwanafunzi.
xi. Pamoja na vifaa tajwa (number i-x), tahasusi zifuatazo wataleta vifaa hivi kwa mchanganuo ufuatao:
    - HKL: Dawa ya chooni aina ya ARO, kwanja moja na watering cane 1
    - HGK: Ufagio wa kukaushia maji (squizer), Ufagio mgumu wa kusugulia sakafu na Panga moja
xii. **Kila mwanafunzi aje na BIMA YA AFYA**; kama hana bima ya afya aje na shilingi 6,000/= kwa ajili ya bima ndogo au shilingi 50,400/= kwa ajili ya Bima kubwa.

**2:3 Michango ya uendeshaji wa shule.**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuchangia Tsh. 80,000/= kwa ajili ya uendeshaji wa shule. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule **50601100156 – Ndago Secondary school A/C – NMB –** (tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye Bank pay in slip) aje nayo anaporipoti shule.
Mchanganuo huo ni kama ifuatavyo:-

| Na | Aina ya mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Michango ya uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

3. **Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi wa mali za shule, mali za watumishi, za jamii na mali za wanafunzi wengine;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni NB: Ndago Sekondari wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;

ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

KARIBU SANA NDAGO SEKONDARI!
**KWETU SISI ELIMU YASHINDA YOTE!**

……………………………………….

**PRISCA TARICHISIO MDEMU**
**MKUU WA SHULE**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZILIZOTAJWA MWANZO WA MAELEKEZO HAYA**

**PRESIDENT'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENTIRAMBA**

**DISTRICT COUNCIL**

NDAGO SECONDARY SCHOOL,
P.O BOX 60,
KIOMBOI-IRAMBA.

________________

To The Medical Officer,

____________________________________

____________________________________

Dear Sir/Madam

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please examine Mr./Miss ……………………………………………………………**.**
as to his/her fitness as a full time student of this school. May I kindly request you to fill in, the particulars given in the form here under.

Yours Sincerely,

……………

**PRISCA TARICHISIO MDEMU**
HEAD MISTRESS

**TO BE COMPLETED BY THE MEDICAL OFFICER**

1. Blood count (White blood cells)…………………………
2. Stool examination ………………………………………..
3. Urine examination………………………………………
4. Gestation (for girl only)…………………………………
5. Venereal diseases…………………………………………
6. T.B test……………………………………………………
7. E.N.T problems……………………………………………
8. Defects of the left and right eye……………………………
9. Defect of the chest………………………………………
10. Does he/she have any CHRONIC or FAMILY diseases Eg. Epilepsy, sickle cell etc.

I have examined Mr. /Miss..............................................................................................and

I certify that he/she is physically **fit/not fit** to pursue student duties as stated above.

……………………………….. ….. ………… ………………

Name and Signature of the medical officer Stamp Date

OFISI YA RAIS

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA SHULE YA SEKONDARI NDAGO**

# FOMU YA HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi ………………………………………………….
2. Tarehe ya Kuzaliwa__________________________wilaya____________________________
3. Mahali alipozaliwa____________________________________________________________
4. Dini (Mkristo/Muislamu)_______________________________________________________
5. Matatizo ya kiafya (kama yapo)__________________________________________________
6. Jina la baba mzazi______________________________yuko hai/amefariki______________
7. Kama amefariki taja mwaka aliofariki_____________________________________________
8. Jina la mama mzazi_____________________________ yuko hai/amefariki______________
9. Kama amefariki taja mwaka aliofariki_____________________________________________
10. Wewe ni mtoto wa ngapi kuzaliwa kwenye familia yenu____________________________
11. Jina la mlezi (kama haulelewi na wazazi)___________________________________________
12. Anuani ya mzazi/mlezi_________________________________________________________
13. Jina la kijiji utokacho__________________________kata_____________________________
14. Kazi afanyayo mzazi/mlezi______________________Namba ya simu___________________
15. Sehemu anakofanyia kazi_______________________________________________________
16. Kazi ambayo ungependa kufanya baada ya kumaliza masomo________________________
17. Habari zingine za jamaa wa familia

| SN | JINA | UHUSIANO | KAZI YAKE | SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |

18. SAINI YA MZAZI/MLEZI________________________________TAREHE__________________

SAINI YA MWANAFUNZI__________________________TAREHE ________________

**OFISI ZA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA**

**SHULE YA SEKONDARI NDAGO**

## SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

**Shule ya sekondari Ndago inaongozwa kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Shule za Sekondari. Aidha, kila mwanafunzi anapaswa kufuata sheria na kanuni zote zilizowekwa wakatiwote uwapo ndani na nje ya shule.**

Kila mwanamafunzi ni lazima atii kanuni na taratibu za shule kwa kuzingatia mambo yafuatayo.

**(i) Nidhamu ni jambo la muhimu kwa kila mwanafunzi. Ili kuonesha nidhamu kilamwanafunzi ni lazima afanye yafuatayo:**

- Kuwa na **Heshima** kwa watu wote, wakubwa kwa wadogo
- Kuwa na **Ushirikiano** na wanafunzi wenzake, walimu, watumishi wasio walimu najamii kwa ujumla.
- Kutokufanya **Makosa** ambayo yanaweza kumsimamisha ama kufutwa shule.
- Kuvaa **Mavazi ya heshima** wakati wote awapo shuleni na nje ya shule.
- Kuwa na **Utii** (kwa amri halali) kwa viongozi, walimu, watumishi wasio walimu,wazazi na jamii kwa ujumla.
- **Utunzaji wa Mali** zake binafsi, na mali za shule
- **Uvumilivu** kwa wanafunzi wenzake, walimu na watumishi wasio walimu.

**(ii) Mahudhurio ni jambo la muhimu pia kwa kila mwanafunzi. Kila mwanafunzianapaswa kufanya yafuatayo:**

- Kutokuwa **mtoro** kwa Kuhudhuria shuleni kila siku (siku 194) za masomo.
- Kutimiza **wajibu** wake kama mwanafunzi awapo shuleni kwa kusoma kwa bidii.
- Kufuata **Ratiba ya shule** wakati wote bila kuzembea.
- **Kuwahi** shuleni kila siku za masomo saa 12:30 asubuhi.
- Kila mwanafunzi anapaswa kutii **Wito wa dharura**, kwa kuhudhuria mahalialipoitwa.

**(iii) Sare za Shule ni jambo la muhimu. Kila mwanafunzi ni lazima:**

- Azingatie kuwa na **Aina sahihi za sare za shule** kama alivyoelekezwa katika barua ya kujiunga na shule.
- Azingatie **Matumizi sahihi ya sare za shule**. Uvaaji wa mlegezo (kata K) hauruhusiwi.
- Azingatie **aina ya Mshono wa sare** ulioelekezwa. Aidha, sketi fupi kwa wasichana haziruhusiwi. Sketi kwa wasichana ni lazima ivuke goti. Ifike angalau sehemu ya mguu kati ya goti na sehemu ya kukanyagia (kiatu).

Suruali za kubana (modal) kwa wavulana haziruhusiwi. Ukibainika umevaa suruali ya kubana, itachanwa kwa mkasi ama wembe.

**(i) Usafi**

- Kila mwanafunzi ni lazima awe **msafi wa Mwili** wakati wote.
- Kila mwanafunzi ni lazima **avae Mavazi safi** wakati wote.
- Kila mwanafunzi ni lazima ahakikishe **Mazingira** (vyumba vya madarasa, vyoo, hosteli, jiko, ofisi za walimu n.k ) ya shule ni safi.

**Yafuatayo ni Makosa Yanayoweza Kusababisha Mwanafunzi Kufukuzwa Shule.**

(i) Wizi
(ii) Kumiliki na kutumia simu bila ruhusa awapo shuleni.
(iii) Uasherati, ubakaji, ushoga, ulawiti na usagaji.
(ii) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya, biashara ya madawa yote ya kulevya.
(iii) Makosa mengine ya Jinai.
(iv) Kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzake, au mtumishi
(v) Kuharibu mali ya umma na ya watu wengine.
(vi) Kudharau Bendera ya Taifa, Picha za viongozi wa Taifa, Nembo ya Taifa, Wimbo waTaifa na fedha za Taifa
(vii) Kuoa au kuolewa.
(viii) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
(ix) Kutoa au kushawishi kutoa mimba.
(x) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
(xi) Kukataa adhabu halali.
(xii) Kujiachisha shule mwenyewe.

---

## KIAPO CHA UTII

Mimi **……………………………………………………….** ambaye ni mwanafunzi wa shule ya sekondari Ndago, nimesoma na kuzielewa sheria, kanuni na taratibu za shule kama zilivyoelezwa hapo juu. Naahidi kwa hiari yangu mwenyewe, nikiwa na akili timamu na bila kushurutishwa na mtu yeyote kuwa **nitatii.** Na endapo nitathibitika kuwa nimekaidi sheria, kanuni na taratibu hizi, uongozi wa shule usisite **kunichukulia hatua stahiki**. Mwenyezi Mungu nisaidie.

| ______________________ | ______________________ | ________________ |
|---|---|---|
| **Jina la mwanafunzi** | **Saini ya mwanafunzi** | **Tarehe** |
| ______________________ | ______________________ | ________________ |
| **Jina la mzazi/mlezi** | **Saini ya mzazi/mlezi** | **Tarehe** |

…………….
**PRISCA TARICHISIO MDEMU**
**MKUU WA SHULE**

(iv) a kutumia simu bila ruhusa awapo shuleni.
(v) Uasherati, ubakaji, ushoga, ulawiti na usagaji.
(xiii) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya, biashara ya madawa yote ya kulevya.
(xiv) Makosa mengine ya Jinai.
(xv) Kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzake, au mtumishi
(xvi) Kuharibu mali ya umma na ya watu wengine.
(xvii) Kudharau Bendera ya Taifa, Picha za viongozi wa Taifa, Nembo ya Taifa, Wimbo waTaifa na fedha za Taifa
(xviii) Kuoa au kuolewa.
(xix) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
(xx) Kutoa au kushawishi kutoa mimba.
(xxi) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
(xxii) Kukataa adhabu halali.
(xxiii) Kujiachisha shule mwenyewe.

---

## KIAPO CHA UTII

Mimi **……………………………………………………..** ambaye ni mwanafunzi wa shule ya sekondari Ndago, nimesoma na kuzielewa sheria, kanuni na taratibu za shule kama zilivyoelezwa hapo juu. Naahidi kwa hiari yangu mwenyewe, nikiwa na akili timamu na bila kushurutishwa na mtu yeyote kuwa **nitatii.** Na endapo nitathibitika kuwa nimekaidi sheria, kanuni na taratibu hizi, uongozi wa shule usisite **kunichukulia hatua stahiki**. Mwenyezi Mungu nisaidie.

| ____________________ | ____________________ | ____________________ |
|---|---|---|
| **Jina la mwanafunzi** | **Saini ya mwanafunzi** | **Tarehe** |
| ____________________ | ____________________ | ____________________ |
| **Jina la mzazi/mlezi** | **Saini ya mzazi/mlezi** | **Tarehe** |

…………….
**PRISCA TARICHISIO MDEMU**
**MKUU WA SHULE**